

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, Changwa Mkwazu, akisoma taarifa ya baadhi miradi ya maendeleo kwa wananchi wa Kata ya Nagaga (hawapo pichani) inayotekelezwa na serikali katika Kata ya Nagaga wilayani Masasi kwenye mkutano na wananchi hao jana. **PICHA: HAMISI NASIRI**

NIPASHE UK 8

# *Wanaoingiza maziwa nchini wasakwa*

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, ametoa mwezi mmoja kwa maofisa wa serikali kuwasaka na kuwakamata watu wanaojihusisha na uingizaji wa mazao ya mifugo nchini, ikiwamo maziwa na kuwachukuliwa hatua kali za kisheria.

Akizungumza wakati wa maadhimisho ya Kilele cha Wiki ya Maziwa yaliyofanyika Kitaifa jijini Dodoma kwa njia ya kielektroniki, Waziri Mpina alisema kamwe Tanzania haiwezi kukubali kugeuzwa soko la bidhaa zinazoingizwa kiholela kutoka nje ya nchi, huku akitaka hatua za kuimarisha uwekezaji nchini ziendelee kuchukuliwa.

Alisema suala hilo litasimamiwa kikamilifu na wizara yake ili kuhamasisha viwanda vya ndani kuongeza uzalishaji na kupunguza uagizaji wa maziwa kutoka nje ya nchi.

Mpina alimwagiza Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo (DVS), Mkurugenzi wa Uzalishaji na Masoko (DPM), Bodi ya Maziwa (TDB) na Bodi ya Nyama (TMB) kuongeza udhibiti kupitia Operesheni Nzagamba, ili kuzuia kwa namna yoyote uingizaji wa mazao ya mifugo nchini bila ya kufuata sheria, kanuni na taratibu.

Pia aliagiza wanunuzi wote wa maziwa hasa wasindikaji kuzingatia mwongozo uliotolewa na wizara wa kununua maziwa ghafi kwa bei isiyopungua Sh. 800 kwa lita ya maziwa, ili kufidia gharama za uzalishaji, kuvutia uwekezaji na kuchochea uzalishaji zaidi kwa wafugaji.

Kadhalika, aliagiza kuzingatiwa bei elekezi ya Sh. 10,000 kwa uhimilishaji kwa ng'ombe bila vichochezi kama ilivyowekwa katika kanuni.

Alisema kanuni hizo zimetungwa ili kuweka usimamizi thabiti wa uhimilishaji nchini na kuweka bei elekezi ambayo inatoa unafuu zaidi kwa wafugaji badala ya kiwango cha zamani cha zaidi ya Sh. 25,000 kwa ng'ombe.

"Ninaagiza katika kipindi cha miaka miwili ijayo nchi yetu isiagize tena maziwa kutoka nje ya nchi, wadau wote wanaagizwa kuweka mikakati madhubuti kufikia malengo hayo," alisema Mpina na kuongeza:

"Nchi yetu ina ardhi yenye rutuba, ina malisho bora na mifugo mingi, hatuwezi kuendelea kuagiza maziwa kutoka nje ya nchi. Tena wakati mwingine tunaagiza maziwa kutoka nchi ambazo hazina hata mifugo, suala hili halivumiliki tena," alisema Waziri Mpina.

Alisema wizara imepokea maelekezo kutoka Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kupitia Mwenyekiti wake, Mahmoud Mgimwa, kupiga marufuku matumizi ya maziwa ya unga kama NIDO, Lactogen kutoka nje ya nchi katika ofisi za serikali.

Alisema suala hilo litasimamiwa kikamilifu na Wizara ya Mifugo ili kuhamasisha viwanda vya ndani kuongeza uzalishaji na kupunguza uagizaji wa maziwa kutoka nje ya nchi.

Msajili wa Bodi ya Maziwa, Dk. Sophia Mlote, alisema wiki ya maziwa imeleta hamasa kubwa kwa wananchi na kumhakikishia Waziri Mpina kuwa atasimamia maelekezo yote ili kuleta mageuzi ya kweli kwenye sekta ya maziwa.

Mwenyekiti wa Baraza la Wadau wa Maziwa, Catherine Dangat, aliishukuru serikali kwa hatua inayochukua ya kudhibiti uingizaji holela wa maziwa kutoka nje ya nchi na kuomba udhibiti huo uendelee ili kulinda viwanda vya ndani.

Scanned with CamScanner




# *Madhara ya kiafya yatokanayo na mabaki ya dawa za mifugo kwenye vyakula vitokanavyo na mifugo*

Immaculata Justin

Mabaki ya dawa za mifugo kwenye vyakula vitokanavyo na mifugo ni kiasi cha dawa inayokuwemo kwenye chakula kitokanacho na mifugo.

Mabaki ya dawa hutokana na dawa za kinga au matibabu zilizotolewa wakati wa uhai wa mnyama au kabla ya kuchinjwa. Kiasi cha dawa hutegemea muda ambao dawa au kinga imetolewa kwa mnyama kabla ya kuchinjwa.

Mtengenezaji wa dawa au chanjo ya mnyama hupendekeza muda maalum wa kutochinja mnyama/mfugo kwa ajili ya kitoweo baada ya mnyama huyo kupatiwa chanjo au dawa ya matibabu.

Tatizo la kuwepo kwa mabaki ya dawa au chanjo za mifugo kwenye bidhaa zinazotokana na mifugo linatokana na wafugaji *kutozingatia muda uliopendekezwa na mtengenezaji wa dawa wa kusubiri au kuacha kuchinja kwa ajili ya kitoweo mnyama ambaye yuko ama alikuwa kwenye chanjo au matibabu.*

*Vyakula au bidhaa za vyakula* vitokanavyo na mifugo ni pamoja na nyama ya ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe na kuku. Vyakula vingine ni pamoja na mayai na maziwa.

**Sababu za kuwepo kwa mabaki ya dawa za mifugo**

- Kutoa chanjo au matibabu kwa mfugo kwa kutumia dawa au chanjo ambazo hazina maelezo (lebo) ya muda maalum wa kusubiri baada ya kutolewa kwa dawa au chanjo kwa mnyama.
- Kutozingatia muda uliopendekezwa wa kuacha kutumia chakula kitokanacho na mifugo kufuatia matibabu au chanjo.
- Utoaji holela wa huduma za matibabu/kinga ya magonjwa ya mifugo.
- Kutoweka kumbukumbu za matibabu na chanjo za mifugo.

**Madhara ya kiafya yatokanayo na mabaki ya dawa za mifugo**

Mabaki ya dawa za mifugo *huweza kusababisha madhara ya kiafya pale mtumiaji wa chakula kitokanacho na mifugo anapokula chakula ambacho kina mabaki juu ya kiwango kinachokubalika.* Viwango vya mabaki ambayo yanakubalika huandaliwa na shirika linalohusika na kuweka viwango vya chakula vya kimataifa "Codex Alimentarius Commission". Madhara hayo ni pamoja na:

Usugu wa vimelea vya magonjwa kwa dawa za binadamu (antibiotics) ambazo zinafanana na zile zilizotumika kutibu mifugo.

Mara nyingi dawa zilizo kwenye kundi moja (antibiotics) hutumika katika matibabu ya wanyama na binadamu. Chanzo kikuu cha usugu wa antibiotics ni kuhamishwa kwa vimelea vya magonjwa ambavyo tayari vimeshakuwa sugu kutoka kwenye mifugo kwenda kwa binadamu kupitia chakula kitokanacho na mifugo ambacho kimechafuliwa na vimelea hao. Mabaki ya dawa za mifugo (antibiotics) yameripotiwa pia kusababisha mazingira ya usugu kwa binadamu.

Mfano dawa inayoitwa tetracycline inatumika kutibu magonjwa yasababishwayo na vimelea aina ya bacteria kwa binadamu. Kwa tiba ya mifugo dawa kama hiyo iitwayo oxytetracycline ambayo hutumika pia kutibu vimelea vya bacteria. Hivyo binadamu ambaye amekuwa akila chakula kitokanacho na mifugo chenye mabaki ya oxytetracycline katika kiwango cha juu ya kile kinachopendekezwa, anapougua huweza kushindwa kupona ugonjwa husika endapo atatibiwa kwa dawa ya tetracycline. Hali hii ya usugu kwa dawa inaweza kugharimu fedha kwa kubadilisha dawa ama kusababisha kifo.

Kusababisha mzio (allergy) kwa baadhi ya watu ambao wana mzio na dawa hizo za mifugo.

Mabaki ya dawa za mifugo kwa baadhi ya dawa ambazo zimepigwa marufuku au kuzuiliwa kutumika yameripotiwa na wanasayansi kuwa na uwezekano mkubwa wa kusababisha saratani; mfano dawa za kundi la Nitrofurans ikiwemo Furazolidone na Nitrofurozone.

Hali kadhalika husababisha kujengeka kwa sumu mwilini.



Mbuzi ni sehemu ya mifugo ambayo inatajwa kuwa mabaki ya dawa zao husababisha athari kubwa za kiafya katika mwili wa binadamu.

**Namna ya kuepuka uwepo wa mabaki ya dawa za mifugo kwenye chakula kitokanacho na mifugo**

Tatizo la uwepo wa mabaki ya dawa za mifugo linaepukika kwa kufanya yafuatayo:-

- Kuzingatia muda wa kusubiri au kutokamua maziwa au kuchinja mfugo ulio kwenye chanjo au matibau kwa mujibu wa maelezo ya mtengenezaji. Kila dawa huwa ina muda wake uliopendekezwa kupita kabla ya kula chakula kutoka kwa mifugo hiyo.
- Kutibu/kukinga mifugo kwa dawa ambazo zina lebo inayoonesha muda wa kuacha kutumia chakula kitokanacho na mifugo kutoka kwa mnyama aliyekuwa kwenye matibabu.
- Matibabu kutolewa na wataalam wa mifugo na kuepuka matumizi holela ya dawa za mifugo.

# Udhibiti wa magonjwa yatokanayo na ulaji wa chakula kisicho salama

Scanned with CamScanner

# Mpina atangaza kibano kwa waagizaji haramu wa maziwa

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina ametoa mwezi mmoja kwa maafisa wa Serikali kuwasaka na kuwakamata watu wote wanaojihusisha na uingizaji wa mazao ya mifugo nchini ikiwemo maziwa na kuwachukuliwa hatua kali za kisheria ili kulinda uwekezaji mkubwa unaoendelea kufanyika nchini kwa sasa.

Pia Wizara imepokea maelekezo kutoka Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kupitia Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa ya kuitaka Serikali kupiga marufuku matumizi ya maziwa ya unga kama NIDO, Lactogen kutoka nje ya nchi katika Ofisi za Serikali.

Waziri Mpina amesema suala hilo litasimamiwa kikamilifu na Wizara yake ili kuhamasisha viwanda vya ndani kuongeza uzalishaji na kupunguza uagizaji wa maziwa kutoka nje ya nchi.

Hivyo katika kipindi hicho cha mwezi mmoja kuanzia sasa amemuagiza Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo (DVS), Mkurugenzi wa Uzalishaji na Masoko (DPM), Bodi ya Maziwa (TDB) na Bodi ya Nyama (TMB) kuongeza udhibiti kupitia Operesheni Nzagamba ili kuzuia kwa namna yoyote uingizaji wa mazao ya mifugo nchini bila ya kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu.

Akizungumza wakati wa Kilele cha Wiki ya Maziwa yaliyofanyika Kitaifa jijini Dodoma kwa njia ya Kielektroniki, Waziri Mpina amesema kamwe Tanzania haiwezi tena kukubali kukubali kugeuzwa soko la bidhaa zinazoingizwa kiholela kutoka nje ya nchi huku akitaka hatua za kuimarisha uwekezaji nchini ziendelee kuchukuliwa. Pia amegiza wanunuzi wote wa maziwa hasa wasindikaji kuzingatia mwongozo uliotolewa na Wizara wa kununua maziwa ghafi kwa bei isiyopungua shilingi 800 kwa lita ya maziwa ili kufidia gharama za uzalishaji, kuvutia uwekezaji na kuchochea uzalishaji zaidi kwa wafugaji.

Mbali na hilo pia ameagiza kuzingatiwa bei elekezi ya shilingi 10,000 kwa uhimilishaji kwa ng'ombe bila vichochezi kama ilivyowekwa katika Kanuni ya Artificial Breeding Regulation 2020 kwani Kanuni hizi zimetungwa ili kuweka usimamizi thabiti wa uhimilishaji nchini na kuweka bei elekezi ambayo inatoa unafuu zaidi kwa wafugaji badala ya kiwango cha zamani cha zaidi ya shilingi 25,000 kwa ng'ombe.

Hivyo Waziri Mpina ameziagiza Sekretarieti zote za Mikoa, Halmashauri zote za Wilaya kuzingatia na kusimamia kikamilifu matumizi ya Bei elekezi kwa chanjo 13 za magonjwa ya kimkakati katika kutoa huduma kwani tayari wizara imeshatangaza Bei elekezi ya chanjo za kimkakati na kusambazwa nchi nzima, hivyo mtu yoyote atakayekiuka achukuliwe hatua kali za kisheria.

Mbali na hilo pia Waziri Mpina amewataka Wafugaji kote nchini kuongeza uzalishaji, kutumia vizuri fursa zinazotolewa na Serikali na kuendelea kuwafuga ng'ombe wa maziwa kwa tija.

Pia Wasindikaji na Wamiliki wa Viwanda wametakiwa kusindika maziwa kulingana na uwezo wa viwanda (Installed capacity) kuliko ilivyo sasa ambapo wanasindika asilimia 23.52 tu ya uwezo wao jambo linalosababisha maziwa mengi kumwagwa kwa kukosa soko na kusababisha maziwa mengi kutokusindikwa jambo ambalo hupelekea kuendelea kutegemea kuagiza maziwa kutoka nje ya nchi.

"Ninaagiza katika kipindi cha miaka miwili ijayo nchi yetu isiagize tena maziwa kutoka nje ya nchi, wadau wote wanaagizwa kuweka mikakati madhubuti kufikia malengo hayo. Nchi yetu ina ardhi yenye rutuba, ina malisho bora na mifugo mingi, hatuwezi kuendelea kuagiza maziwa kutoka nje ya nchi. Tena wakati mwingine tunaagiza maziwa kutoka nchi ambazo hazina hata mifugo, Suala hili halivumiliki tena," alisema waziri Mpina

## Wakulima wapewa mwezi mmoja ..

alivitaka vyombo vya ulinzi na usalama kushirikiana na TFS kuwadhibiti na kuwachukulia hatua kali za kisheria wakulima ambao ni Watanzania wanaotoa kazi za vibarua ambao ni raia wa Burundi kulima ndani ya msitu huo.

Aliitaka TFS kuwakamata vibarua hao ambao sio raia wa Tanzania na kuwapeleka mahakamani hatua ambayo itasaidia kuwataja Watanzania wanaotoa vibarua vya kulima katika msitu huo kwa wageni.

Kwa upande Mbunge wa Kasulu Vijijini, Vuma Ole alisema, hatua ya kuwaruhusu wananchi kuvuna mazao yao itasaidia kupunguza uhasama uliopo baina ya wakulima na wahifadhi.

Hata hivyo, aliitaka TFS kusimamia msitu wa Makere kipindi chote na sio kipindi cha mavuno pekee kwani hali hiyo inashawishi mazingira ya rushwa.

Awali Mkuu wa Wilaya ya Kasulu, Kanali Saimon Anange alisema, baada ya kuchunguza malalamiko yanayotolewa na wananchi imebainika kuwa wakulima wengi wanaolima katika msitu huo ni raia wa Burundi na sio Watanzania kama inavyodaiwa.

Kutokana na hali hiyo, Kanali Anange aliwaonya Watanzania wanaowakaribisha raia hao wa Burundi na kuwapa vibarua vya kulima katika msitu huo waache mara moja.

Kwa upande wake, Mhifadhi Mkuu wa TFS, Prof.Dos Santos Silayo aliwataka wananchi kufuata



Mstahiki Meya

# BODI YA MAZIWA TANZANIA

## HOTUBA YA MHESHIMIWA LUHAGA JOELSON MPINA (MB.), WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI KATIKA KILELE CHA MAADHIMISHO YA WIKI YA MAZIWA YALIYOFANYIKA KITAIFA MKOANI DODOMA KWA NJIA YA KIELEKITRONIKI, TAREHE 04 JUNI, 2020




Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Joelson Mpina







kunachosimamia
wa kwa wananchi
wenda ACT miaka
apt walihoji wa-

...kijamii na hata kisiasa
ambapo amewataka wajipange ka-
tika uchaguzi mkuu kuhakikisha
serikali ya umoja wa kimataifa kina-
shiriki kikamilifu.

PICHA: MPIGAPICHA WETU



...dhi vifaa saidizi
... (kulia) vilivyo-
...oto) kwa ajilli ya

# ... Kolo

...ale huku akidai
...tokea sababu ya
...a watu weusi wa-
...wataka Watanza-
...eneo la michoro
...loa na kuangalia
...yopo pamoja na
... kupanda mlima.
...je hapa mimi ni-
... kuja na familia
...a mkafanya ma-
...uu mlima huku
...o na gharama ni

...o cha Michoro
... Kondoa,Zubeir
...o hilo ni kielel-
...a kale ambapo
...angi ndio lenye
...di.
...ro, imechorwa
...ima na waokota
...a wakiishi ka-

MTANZANIA UK9.

## MKAKATI

DODOMA

# Serikali kutokomeza magonjwa 'sumbufu' kwa mifugo nchini

**Na MWANDISHI WETU**

SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeweka mkakati madhubuti wa kutokomeza Magonjwa yanayoandama mifugo ili kuwa na mifugo bora itakayozalisha kwa tija na kukuza uchumi wa nchi.

Kauli hiyo, ilitolewa na Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo wa Tanzania, Profesa Hezron Nonga wakati mkutano wa 45 wa Baraza la Veterinari uliofanyika jijini Dodoma.

Akizungumza na Waandishi wa habari mara baada ya mkutano huo, Profesa Nonga alisema Tanzania kuna mifugo takriban milioni 34, pamoja na wingi huo wa mifugo bado nchi haijafikia uzalishaji mkubwa kutokana na magonjwa yanayoandama mifugo hiyo.

Alisema maka 2018, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, iliamua kuja na mkakati wa kufanya mageuzi makubwa katika huduma za mifugo upande wa afya ili kuwa na mifugo bora itakayotoa mazao bora na salama kwa matumizi ya binadamu. Alisema mkakati huo, umejikita zaidi kukinga mifugo dhidi ya magonjwa umeweka utaratibu wa kuhakikisha mifugo yote inaogeshwa na kupata chanjo stahiki dhidi ya magonjwa ya kipaumbele.

Magonjwa yanayochangia kukwamisha uzalishaji wenye tija kwa mifugo,ni ugonjwa wa miguu na midomo, Ndiganakali na mapele ngozi.

"Lengo letu ni kuhakikisha mifugo yote inapata chanjo kulingana na kalenda ya uchanjaji ili kuwakinga na magonjwa hayo sumbufu", alisema Profesa NongaAlisema mkakati huo umepanga kuwa katika kila kijiji,kata, wilaya hadi mkoa kuwe na majosho ya kuogeshea ng'ombe na mifugo mingine walau mara mbili kwa mwaka ili kuwalinda na maradhi yanayosababishwa na Kupe pamoja na wadudu wengine.

Scanned with CamScanner

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# Wizara ya Mifugo na Uvuvi

## HOTUBA YA MHESHIMIWA LUHAGA JOELSON MPINA (Mb.), WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI KWENYE KILELE CHA MAADHIMISHO YA WIKI YA MAZIWA YALIYOFANYIKA KITAIFA MKOANI DODOMA KWA NJIA YA KIELEKITRONIKI, TAREHE 04 JUNI, 2020




**Mhe. Mahmoud Mgimwa (Mb.), Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya kilimo, Mifugo na Maji;**

**Mhe. Dkt. Binilith Mahenge, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma ambaye amewakilishwa na Mhe. Patrobas Katambi, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma;**
**Bi. Catherine Dangat, Mwenyekiti wa Baraza la Wadau wa Maziwa;**

**Prof. Davis Mwamfupe, Mstahiki Meya;**

**Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya;**
**Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Wilaya;**
**Wakurugenzi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi;**
**Dkt. Sophia Mlote, Kaimu Msajili wa Bodi ya Maziwa Tanzania;**
**Wadau wa Tasnia ya Maziwa;**
**Taasisi za Kifedha;**
**Wataalam wa Sekta ya Mifugo mliopo hapa;**
**Waandishi wa Habari; Wageni Waalikwa;**
**Ndugu Wananchi; Mabibi na Mabwana.**

Napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na kutuwezesha kuiona siku ya leo licha ya changamoto kubwa ya ugonjwa wa COVID -19 uliosababishwa na Virusi vya CORONA unaoikabili dunia kwa sasa. Kipekee, nashukuru Baraza la Wadau wa Tasnia ya Maziwa kwa kunialika ili nishiriki siku hii muhimu ya Kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Maziwa kitaifa. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Bodi ya Maziwa Tanzania; Wazalishaji na Wasindikaji wa Maziwa; Taasisi za Serikali na Mashirika yasiyo ya Kiserikali na Washirika wa Maendeleo ya Tasnia ya Maziwa nchini kwa kuandaa siku hii muhimu ambayo ni ya kwanza na ya kipekee kuadhimishwa kwa njia ya kielekitroniki.

**Mabibi na Mabwana**, Nichukue nafasi hii kuwasihi watanzania wenzangu kama Rais Wetu, **Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli** alivyotuelekeza kuendelea kuchapa kazi huku tukichukua tahadhari zote tunazoelekezwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na vyombo vyetu vya usalama huku tukimtanguliza Mungu wetu.

**Mabibi na Mabwana**, wazungumzaji walionitangulia Msajili wa Bodi ya Maziwa, Chama cha Uzalishaji wa Maziwa Tanzania (TAMPRODA), Chama cha Wasindikaji wa Maziwa (TAMPA), Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Mhe. Patrobas Katambi wameongea mengi kuhusu Taarifa ya maadhimisho ya 23 ya Wiki ya Maziwa ambapo fursa na changamoto zimeelezwa kwa kina na kuweka mwelekeo sahihi katika kilele cha maadhimisho haya.

**Mabibi na Mabwana,** kama mtakavyokumbuka Maadhimisho haya yalianzishwa Mwaka 2001 na Shirika la Kimataifa la Kilimo na Chakula (FAO) na Shirika la Afya Duniani (WHO) baada ya kuombwa na nchi wanachama ambao waliona umuhimu wa viinilishe vilivyomo kwenye maziwa kwa afya ya binadamu na hivyo kutaka kila nchi ijitegemee na kujitosheleza kwa uzalishaji na utumiaji wa maziwa kwa kuadhimisha kimataifa.

**Mabibi na Mabwana,** Maziwa ni mlo kamili na chakula cha kipekee chenye viinilishe vyote muhimu kwa mwili wa binadamu ambavyo vinamuwezesha kufanya shughuli zake za kila siku kwa ufanisi. Maziwa yana protini, wanga, mafuta, maji, vitamin A, B1, B2, B6 na madini mbalimbali kama ***calcium*** na ***phosphorus***. Madini haya ni muhimu sana hasa katika kuimarisha mifupa na ubongo kwa rika zote. Aidha, maziwa yana viinilishe ambavyo vinaimarisha kinga na afya ya mwili hususan kwa kipindi hiki ambacho dunia imekumbwa na janga la ugonjwa wa COVID – 19. Viinilishe vyote hivi, vinapatikana kwa pamoja na kwa uwiano unaotakiwa. Hivyo, maziwa ni chakula kamili kinachojitosheleza kwa afya ya binadamu.

**Mabibi na Mabwana**, nchi yetu ina ng'ombe **milioni 33.4** na ni nchi ya pili baada ya Ethiopia yenye ng'ombe **milioni 54** kwa Afrika kuwa na ng'ombe wengi. Kati ya hao, ng'ombe **milioni 1.95** ni ng'ombe wa maziwa. Ng'ombe hawa kwa ujumla wanazalisha maziwa lita **bilioni 3.01** ambapo lita **bilioni 2.1** zinatokana na ng'ombe wa asili na lita **bilioni 0.91** zinatokana na ng'ombe wa kisasa.

**Mabibi na Mabwana**, pamoja na kwamba nchi yetu ni ya pili kwa nchi za Afrika kuwa na ng'ombe wengi, bado ng'ombe wa maziwa ni wachache na pia uzalishaji wa maziwa ni kidogo. Unywaji wa maziwa unaoshauriwa na Shirika la Chakula Duniani kwa mtu kwa mwaka ni **lita 200** lakini hali halisi ya kila mtanzania kwa mwaka anakunywa wastani wa **lita 54.7** tu sawa na **asilimia 27** ya lengo.

**Mabibi na Mabwana,** tasnia ya maziwa bado tupo nyuma ikilinganishwa na majirani zetu, usindikaji wa maziwa ni **asilimia 2.7** ya maziwa yanayozalishwa nchini huku **asilimia 93.3** ikitumika ikiwa ghafi katika familia, na kuuzwa katika vioski na maduka. Viwanda vya kusindika maziwa vinasindika asilimia 23 tu ya uwezo wake huku upande wa wafugaji wakimwaga maziwa kwa kukosa soko. Vilevile, bei ya maziwa katika masoko yasiyo rasmi ni kubwa kuliko inayotolewa na viwanda.

**Mabibi na Mabwana**, Mpaka sasa kuna program za unywaji maziwa shuleni katika mikoa ya Iringa, Njombe, Arusha, Tanga, Kilimanjaro, Morogoro na Dar es Salaam ambapo wanafunzi **64,655** kutoka shule zaidi **145** wananufaika na mpango huu. Hivyo, nahamasisha programu hizi zifanyike nchi nzima ili kuongeza unywaji wa maziwa. Aidha, Bodi ya Maziwa inafanya kampeni za unywaji maziwa kwa kushirikiana na sekta binafsi kupitia maonesho mbalimbali ikiwa ni pamoja na SabaSaba, NaneNane, Siku ya Unywaji Maziwa Shuleni ambapo mwezi Septemba, 2019 ilifanyika mkoani Iringa na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuwa mgeni rasmi. Katika maadhimisho hayo, shule **10** zenye wanafunzi zaidi ya **3,000** na wananchi zaidi ya **7,000** walishiriki. Vilevile, uhamasishaji wa unywaji maziwa unafanyika katika Wiki ya Maziwa.

**Mabibi na Mabwana**, nchi yetu ina **viwanda 99** vinavyosindika maziwa na kati ya hivyo ni **viwanda 5** tu vina uwezo wa kusindika zaidi ya **lita 5,000** kwa siku na **viwanda 94** vinasindika chini ya **lita 5,000**. Nitoe wito kwa wawekezaji nchini kuwekeza katika viwanda vya kusindika maziwa na kuongeza kiwango cha kusindika kwa siku ili kufikia uchumi wa kati ifikapo Mwaka 2025. Uwezo uliosimikwa kwa viwanda hivi ni **lita 865,600** kwa siku sawa na **lita milioni 74,314,000** kwa mwaka. Kwa sasa vinasindika **lita 203,600** kwa siku sawa na **asilimia 23.52**. Natoa wito kwa viwanda vyote nchini kusindika kulingana na uwezo uliosimikwa.

Scanned with CamScanner

Guardian VOTED Superbrands East Africa's Choice 2019-2020

The Guardian
www.ippmedia.com

pestguard
Professional Pest Control Services
FUMIGATION SERVICES
Export Containers and Warehouses using Methyl Bromide and Phosphine
+255 658 781861/ 022 2123565
www.pestguard.co.tz

theguardiantz theguardianltd The Guardian Digital +255 745 700 710 LIKE & FOLLOW US

ISSN 0856 - 5422 ISSUE No 7922 • PRICE Tsh 1,000, Kenya sh100 TANZANIA MONDAY 8 JUNE, 2020

National Pg 3
AG identifies weaknesses in by-laws



National Pg 4
Govt all out to provide lifeboats



National Pg 5
Investment climate for businesses



tnbc

National Pg 6
TAMWA empowers Z'bar GBV victims

STOP GENDER-BASED VIOLENCE



## 'TCB, not govt to set cotton prices'

By Guardian Correspondent, Mwanza

AGRICULTURE minister Japhet [H]asunga has said the government will not [b]e involved in setting up cotton prices, [s]aying it will be determined by the market.

The minister (pictured) was speaking [h]ere yesterday at a meeting of cotton [st]akeholders from 17 regions grouping 56 [d]istricts growing the crop.

He said that the task of setting up cotton [p]rices will be carried out by the Tanzania [C]otton Board (TCB).

"When you leave prices to be [d]etermined by the market, farmers have [t]o be adequately educated to know the [p]rice applicable for that year. For the [w]hole of last year the agricultural sector [c]ontributed 28.7 percent to GDP," he [p]ointed out.

"Our role as government is to ensure [th]at the crop meets the required standards [an]d ensure that the market is available," [he] said.

He also pointed at the need for [ca]pacitating local industries to use locally [gr]own cotton and export processed [go]ods rather than raw materials, adding:

> "Our role as government is to ensure that the crop meets the required standards and ensure that the market is available

[Th]is will help the country do away with [imp]orted second hand clothing."

[C]otton production has increased from [...]78 tonnes in the 2015/2016 season to [...]910 in the 2019/2020 season.

[Ac]hievements recorded in cotton [pro]duction were stimulated by [impr]ovements in the wider agricultural [sect]or, including proper usage of [pesti]cides, steady supply of quality seeds [and i]nputs.

[In] the 2018/19 farming season, farmers [us]ed certified and improved seeds such [as U]KM08, which is highly productive.

[Th]e target is to produce one million [tonn]es of cotton by 2022/2023, the [mini]ster noted.

[W]e've also changed the cotton [purc]hasing system and currently the crop [is so]ld through Agricultural Marketing [Coop]erative Unions (AMCOs) instead of [...]s purchasing directly from farmers.

# Mineral dealers to do business outside hubs



Livestock and Fisheries minister Luhaga Mpina (2nd-L) and other dignitaries including Dodoma district commissioner Patrobas Katambi, Tanzania Dairy Board registrar Dr Sophia Mlotte and Dodoma City mayor Prof Davis Mwamfupe drink milk at Dairy Week event in Dodoma yesterday. Photo: Guardian Correspondent

By Guardian Correspondent, Geita

THE government has temporarily allowe[d] mineral dealers to procure minerals outsid[e] officially established trading centres followin[g] trading challenges in the wake of the nov[el] coronavirus outbreak.

Minerals minister Doto Biteko told traders [of] minerals in Geita Region that the permissi[on] will be reviewed after three months.

The decision is meant to boost governm[ent] revenues from the sector despite the pande[mic] being around, as well as helping to stimul[ate] other economic activities generally, he said.

The minister had earlier visited proj[ects] implemented by the Geita Gold Mining [...] (GGML) in corporate social responsibility (C[SR]) initiatives.

He urged traders to only make sure they h[ave] all the required permits indicating where [the] minerals have been bought from and wh[ere] they will be sold.

"Minerals sector contribution in reve[nue] collection is enormous. We want to see to it [that] the business stimulates economic activity[," he] emphasised.

He said that the government's intenti[on is] to see areas with mineral resources incl[uding] Geita transform people's lives and the eco[nomy] of the surrounding communities.

"I am impressed by the way govern[ment] authorities in Geita manage revenue coll[...]

TURN TO [...]

## Govt pounces on cattle, dairy product imports

■ Public agencies to source milk from local producers

By Guardian Correspondent, Dodoma

THE government has announced a one-month crackdown on illegal importers of livestock and dairy products to control rampant smuggling and protect local producers.

Livestock and Fisheries minister Luhaga Mpina said here yesterday that to further boost the market for local products, government agencies and institutions have been restricted from using imported milk powder.

The ban on the use of imported milk powder was recommended in a recent report of the Parliamentary Standing Committee on Agriculture, Livestock and Water.

It is expected to increase local production of dairy products and protect investors, he stated.

Officiating at the national milk week climax, the minister tasked the Tanzania Dairy Board (TDB), the Tanzania Meat Board (TMB), the director of Veterinary Services and the director of production and markets to further intensify controls through 'Operation Nzagamba'.

"There should be no more smuggling of livestock and dairy products after one month. We are making huge investments in the dairy-sub sector, so we can produce enough products for

TURN TO PAGE 2

## SHARE FACTS ABOUT COVID-19

Know the facts about coronavirus disease 2019 (COVID-19) and help stop the spread of ru[mors]

**FACT 1** Diseases can make anyone sick regardless of their race or ethnicity.

Fear and anxiety about COVID-19 can cause people to avoid or reject others even though they are not at risk for spreading the virus.

**FACT 2** For most people, the immediate risk of becoming seriously ill from the virus that causes COVID-19 is thought to be low.

Older adults and people of any age who have serious underlying medical conditions may be at higher risk for more serious complications from COVID-19.

**FACT 4** There are simple things y[ou can] do to help keep yourself [and] others healthy.

- Wash your hands often with so[ap] and water for at least 20 secon[ds], especially after blowing your n[ose], coughing, or sneezing; going [to] the bathroom; and before eat[ing or] preparing food.
- Avoid touching your eyes, no[se, and] mouth with unwashed hand[s].
- Stay home when you are sic[k].
- Cover your cough or sneeze [with a] tissue, then throw the tissue [in] the trash.

Scanned with CamScanner